# JARIDA LA HABARI

ISO:9001 2015 Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA)

TOLEO NAMBA: 003 OKTOBA, 2019 www.meteo.go.tz


## TMA YATOA MWELEKEO WA MVUA ZA VULI 2019




uk 5

# TMA YAZINDULIWA RASMI



Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Mhe. Mhandisi Isack Kamwelwe akizungumza wakati wa uzinduzi rasmi wa TMA kutoka kuwa Wakala (Agency) katika ukumbi wa Ubungo Plaza, Dar es Salaam

# MAMLAKA YA HALI YA HEWA YAZINDULIWA RASMI




**Katibu Mkuu, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Dkt. Leonard Chamuriho akizungumza wakati wa uzinduzi rasmi wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) kutoka kuwa Wakala (Agency) katika ukumbi wa Ubungo Plaza, Dar es Salaam**



**Kamati ya hafla ya uzinduzi katika picha ya pamoja na mgeni rasmi wakati wa uzinduzi rasmi wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) kutoka kuwa Wakala (Agency) katika ukumbi wa Ubungo Plaza, Dar es Salaam**




**Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya TMA iliyomaliza muda wake Dkt. Buruhani Nyenzi akizungumza wakati wa uzinduzi rasmi wa TMA kutoka kuwa Wakala(Agency) katika ukumbi wa Ubungo plaza, Dar es salaam**



**Mkurugenzi Mkuu TMA na Makamu wa tatu Rais wa WMO Dkt. Agnes Kijazi akizungumza wakati wa uzinduzi wa TMA kutoka Wakala (Agency) katika ukumbi wa Ubungo plaza, Dar es salaam**

**Tarehe 05/09/2019: Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Mhe. Mhandisi Isack Kamwele amezindua rasmi Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) kutoka kuwa Wakala (Agency) katika ukumbi wa Ubungo Plaza, Dar es Salaam.**

Uzinduzi wa Mamlaka umetokana na sheria ya Mamlaka ya Hali ya Hewa "Tanzania Meteorological Authority Act No.2 of 2019" iliyopitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kusainiwa tarehe 13 Februari, 2019 na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, awali Wakala huo ulianzishwa baada ya iliyokuwa Idara Kuu ya Hali ya Hewa kubadilishwa na kuwa Wakala wa Serikali mnamo mwaka 1999 kwa Sheria yaw akala wa Serikali sura 245 marejeo ya 2002.

Idara Kuu ya Hali ya Hewa (Directorate of Meteorology) ambayo ilianzishwa mwaka 1977 baada ya kuvunjika kwa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, ilikuwa na jukumu la kuangaza na kutoa taarifa za hali ya hewa nchini. Kabla ya hapo huduma hizo zilikuwa zikitolewa na Idara ya Hali ya Hewa ya Afrika Mashariki (EAMD).

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, Mhe. Kamwelwe aliwajulisha washiriki kwamba ndege yetu iliyokuwa inashikiliwa Afrika Kusini imekwishawasili nchini baada ya Serikali kushinda kesi. Mheshimiwa Kamwelwe alimpongeza Mkurugenzi Mkuu wa TMA Dkt. Agnes Kijazi kwa kuchaguliwa kuwa Makamu wa Tatu wa Rais wa Shirika la Hali ya Hewa Duniani.

Aidha, alimpongeza Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya TMA, Dkt. Buruhani Nyenzi kwa usimamizi mzuri wa Mamlaka. Akizungumzia uzinduzi wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania Mheshimiwa Kamwelwe alisema Wakala wa Hali ya Hewa Tanzania 'Tanzania Meteorological Agency' imepandishwa hadhi na kuwa Mamlaka, hivyo kuweza kukidhi pande zote mbili za Tanzania Bara na Visiwani

Wakati akitoa neno la ukaribisho, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo Dkt. Leonard Chamuriho alisema huduma za hali ya hewa ni mtambuka zinahitajika katika sekta zote ikiwemo ya viwanda, kwa hiyo wageni wote waalikwa wako katika uzinduzi huo kutokana na umuhimu wa huduma hizo za hali ya hewa

Aidha, wakati akiwasilisha taarifa ya uzinduzi TMA na mifumo mbalimbali ya kiutendaji, Mkurugenzi Mkuu wa TMA Dkt. Agnes Kijazi alielezea kuwa Mamlaka imeongezewa jukumu la kudhibiti na kuratibu utoaji na utumiaji wa huduma za hali ya hewa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na alikabidhi hati kutoka Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO) za kutambua rasmi vituo vya Songea na Bukoba kuwa na takwimu za muda mrefu za zaidi ya miaka 100.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Ndugu. Mustafa A. Jumbe aliwasisitiza kuwa hali ya hewa haina mipaka na kudhihirisha jinsi Tanzania Visiwani wanavyozingatia tahadhari zinazotolewa na TMA kwa usafiri wa baharini.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya TMA, Dkt. Buruhani Nyenzi alielezea mafanikio ya uongozi wa Bodi anayoiongoza ikiwa ni kupatikana kwa sheria iliyopelekea kuzindua Mamlaka hiyo.

Uzinduzi huo ulihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa serikali, wakurugenzi wa taasisi, wawakilishi wa sekta binafsi, asasi za kiraia, mashirika ya kimaendeleo, wanahabari na wafanyakazi wa TMA. Ulienda sambamba na uzinduzi wa nembo mpya, tovuti mpya na mifumo ya "TMA Digital Meteorological Observatory (TMA-DMO)" kwa ajili ya kurahisisha mawasiliano ya Data za Hali ya Hewa; "Meteorological Aviation Information System (MAIS)" kwaajili ya kurahisisha utoaji wa huduma za hali ya hewa katika usafiri wa anga na " Marine Meteorological Information System (MMIS)" unaosaidia sana katika utoaji wa huduma za hali ya hewa kwa sekta ya kwenye maji yaani bahari, maziwa na mito

JARIDA LA HABARI
ISO: 9001 2015 Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga
Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA)

Jarida hili limeandaliwa na

**Mhariri -** Dkt. Agnes Kijazi

**Mwandishi -** Monica Mutoni , **Msanifu Kurasa -** Ikupa Mwakiteleko



Wadau wa Maendeleo katika picha ya pamoja na mgeni rasmi wakati wa uzinduzi rasmi wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) kutoka kuwa Wakala (Agency) katika ukumbi wa Ubungo Plaza, Dar es Salaam




Wajumbe wa Bodi ya Ushauri ya TMA iliyomaliza muda wake, katika picha ya pamoja na mgeni rasmi wakati wa uzinduzi rasmi wa TMA kutoka kuwa Wakala(Agency) katika ukumbi wa Ubungo Plaza, Dar es Salaam



Mkurugenzi Mkuu wa TMA akikabidhi cheti cha shukrani ya kutambua mchango wa bodi iliyomaliza muda wake wakati wa uzinduzi rasmi wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) kutoka kuwa Wakala (Agency) katika ukumbi wa Ubungo Plaza, Dar es Salaam




Wawakilishi wa Wizara mbalimbali za Serikali katika picha ya pamoja na mgeni rasmi wakati wa uzinduzi rasmi wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) kutoka kuwa Wakala (Agency) katika ukumbi wa Ubungo Plaza, Dar es Salaam









# DKT. KIJAZI MAKAMU WA TATU WA RAIS WA WMO



'Napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru wote waliokuwa pamoja na mimi kwa kuniunga mkono na kunichagua kwa kura zote, naahidi kuitumikia nafasi hii kwa weledi mkubwa na kuhakikisha WMO inafikia malengo yake'.

**Kwa mara nyingine Tanzania imeingia katika historia ya kimataifa kwa Mkurugennzi Mkuu wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania na mwakilishi wa kudumu Tanzania katika Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO) kuibuka mshindi wa nafasi ya umakamu wa tatu wa Rais wa WMO. Dkt. Kijazi anachukua nafasi hiyo kwa kipindi cha miaka minne kuanzia 2019-2022 akiwa mwanamke wa kwanza na mjumbe wa kwanza kutoka nchi zinazoendelea kushika nafasi hiyo. Dkt. Kijazi atakuwa na majukumu makubwa ya kumsaidia Rais kuongoza shirika hilo katika kutekeleza majukumu yenye tija kwa wanachama wake ikiwemo Tanzania**

Akizungumzia ushindi wake mbele ya wapiga kura wa mkutano wa 18 wa Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO) na wajumbe waalikwa, Dkt. Kijazi alitoa shukrani zake za dhati kwa wote waliomwamini na kumuunga mkono hadi kufika kupata nafasi hiyo na kuahidi kuitumikia nafasi hiyo kwa weledi wa hali ya juu ili kufikia malengo ya shirika hilo.

'Napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru wote waliokuwa pamoja na mimi kwa kuniunga mkono na kunichagua kwa kura zote, naahidi kuitumikia nafasi hii kwa weledi mkubwa na kuhakikisha WMO inafikia malengo yake'. Alisema Dkt Kijazi

Akizungumzia ushindi huo, Naibu Waziri wa Uchukuzi na Mawasiliano Dkt. Atashasta Nditiye alisema ni heshima kubwa sana kwa nchi, Wizara inampongeza sana Dkt. Kijazi na kuamini kuwa ataiwakilisha nchi vizuri, aidha alimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ushirikiano aliouonesha kwa kukubali Tanzania kuwakilishwa na Dkt. Kijazi ambapo kwa jitihada zake katika kuboresha sekta ya hali ya hewa kumeendelea kuiletea sifa nchi kwa ujumla

Kwa upande wa Kaimu Balozi, Ubalozi wa Kudumu Umoja wa Mataifa, Geneva Ndugu. Robert Kahendaguza alisema kuwa ushindi wa Dkt. Kijazi ni kielelezo cha umadhubuti wa kidiplomasia ya Tanzania na sifa zake binafsi ikiwemo uzoefu wa muda mrefu na elimu ya ngazi ya juu katika nyanja ya sayansi ya hali ya hewa, aidha aliongeza kuwa sababu za sifa hizo ziliupunguzia ubalozi kazi ya kumnadi na hata kuwa rahisi kuishawishi nchi ya Sudan kuondoa mgombea wao na hivyo kumfanya Dkt. Kijazi kuwa mgombea pekee katika uchaguzi huo.

Uchaguzi wa viongozi wa WMO hufanyika kila baada ya miaka minne kwa kuchagua viongozi mbali mbali wakiwemo Katibu Mkuu, Rais, Makamu wa Rais wa kwanza, wa pili na wa tatu, ambapo kwa mwaka huu umefanyika katika mkutano wa 18 wa shirika hilo baada ya muda wa viongozi hao kuisha. Uchaguzi huo ulifanyika kwa haki na kwa amani na kuwapata viongozi hao ambao ni Prof. Petteri Taalas kutoka Finland (Katibu Mkuu), Prof. Dk. Gerhard Adrian kutoka Ujerumani (Rais), Prof. Celeste Saulo kutoka Argentina (Makamu wa kwanza wa Rais), Dr. Albert Martis kutoka Curacao (Makamu wa Pili wa Rais) na Dkt. Agnes Kijazi kutoka Tanzania (makamu wa tatu wa Rais).





Mkurugenzi mkuu wa TMA na Makamu wa tatu wa Rais wa Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO) Dkt. Agnes Kijazi, mbele ya waandishi wa habari akichambua mwenendo wa mifumo ya hali ya hewa na mwelekeo wa mvua

# TMA YATOA MWELEKEO WA MVUA ZA VULI 2019

Tarehe 03/09/2019:Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) imetoa rasmi utabiri wa msimu mvua wa kuanzia mwezi Oktoba 2019 hadi Desemba, 2019. Taarifa hiyo imetoa uchambuzi wa mwenendo wa mifumo ya hali ya hewa na mwelekeo wa msimu wa mvua katika kipindi cha mwezi Oktoba hadi Desemba, 2019 sambamba na ushauri na tahadhari kwa wadau wa sekta mbali mbali.

Akizungumza na waandishi wa habari, Mkurugenzi Mkuu wa TMA, Dkt. Agnes Kijazi aliezea kuwa Utabiri huo ni mahsusi kwa maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka ambayo ni nyanda za juu kaskazini mashariki, Pwani ya kaskazini, Ukanda wa Ziwa Viktoria pamoja na kaskazini mwa mkoa wa Kigoma .




Aliendelea kwa kusema kuwa, maeneo yanayozunguka ukanda wa Ziwa Viktoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Mwanza, Shinyanga, Simiyu na Mara) yanatarajiwa kuwa na mvua za wastani hadi juu ya wastani. Aidha maeneo mengine yaliyosalia (Pwani ya Kaskazini pamoja na Nyanda za juu kaskazini Mashariki), mvua zinatarajiwa kuwa za wastani hadi chini ya wastani ambapo maeneo ya ukanda wa Ziwa Viktoria mvua zinatarajiwa kuanza katika wiki ya pili ya mwezi Oktoba, 2019 isipokuwa maeneo machache ya mkoa wa Kagera ambapo vipindi vya mvua za nje ya msimu zilizoanza toka mwezi Agosti 2019, vinatarajiwa kuendelea na hivyo kuungana na kuanza kwa msimu wa mvua za Vuli.

Akielezea athari zinazotarajiwa ni pamoja na maeneo yanayotarajiwa kupata mvua nyingi kuna uwezekana wa matukio ya magonjwa ya mlipuko yanaweza kujitokeza, hali kadhalika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za wastani hadi chini ya wastani magonjwa ya mlipuko pia yanaweza kujitokeza kutokana na uhaba wa maji safi na salama, vilevile upungufu wa malisho hususani katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za wastani hadi chini ya wastani unaweza kujitokeza. Hali hiyo inaweza kusababisha migogoro kati ya wakulima na wafugaji.

Alimalizia kwa kuwataka wananchi kuendelea kufuatilia taarifa za hali ya hewa zinazotolewa na TMA sambamba na kuchukua tahadhari ya vipindi vifupi vya mvua kubwa vinavyotarajiwa kujitokeza katika baadhi ya maeneo.

# BALOZI SEIF AFURAHISHWA NA HATUA YA TMA KUANZA KUTEKELEZA MKATABA WA KUSITISHA MATUMIZI YA ZEBAKI NCHINI







**Tarehe 20/09/2019:** "Nimefurahi kusikia Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) imeanza kutelekeza mkataba wa MINAMATA wa kusitisha matumizi ya zebaki katika vifaa vya hali ya hewa", alizungumza Mhe. Balozi Seif Ali Iddi, Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, mara baada ya kufunga mkutano wa mawaziri wa SADC wa sekta ya tehama, habari, uchukuzi na hali ya hewa na kutembelea banda la TMA kwenye ukumbi wa mikutano wa kimataifa wa Mwl. Julius Nyerere, Dar es Salaam.

Naye, Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhe. Mhandisi Isack Kamwelwe alimueleza Mhe. Balozi Seif kuwa serikali inaangalia namna sahihi ya kuweze kuteketeza vifaa hivyo kiusalama Zaidi, kwa vile zebaki ni moja ya vitu vinavyochangia katika uharibifu wa mazingira.

Kwa upande wa Mkurugenzi wa Huduma za Utabiri ambaye pia ni Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TMA, Dkt. Hamza Kabelwa alisema kuwa, TMA imeshafanikisha zoezi hilo la kuacha matumizi ya vifaa vyenye zebaki vikiwemo vipima joto (thermometers), vipima mgandamizo wa hewa (barometers) n.k kwa asilimia kubwa kwa kuwezeshwa na serikali upatikanaji wa vifaa ambavyo havitumii zebaki.

Mkutano huo umefungwa rasmi leo tarehe 20 Septemba 2019. Kauli mbiu ya mkutano huo ilikuwa ***'Mazingira Wezeshi kwa Ukuaji wa Uchumi Jumuishi na Endelevu, Kukuza Biashara katik Jumuiya na Kuongeza Fursa ya Ajira'***

# WAZIRI KAMWELWE AHIMIZA MIPANGO MADHUBUTU YA KUKABILIA NA ATHARI ZA MABADILIKO YA HALI YA HEWA



Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Isaack Kamwelwe aki-fungua mkutano wa 53 wa utabiri wa msimu wa vuli kwa nchi 11 za pembe ya Afrika unaofanyika kwenye hoteli ya Hyatt Regency jijini Dar



Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), Dk. Agnes Kijazi akizungumza katika mkutano huo unaofanyika kwenye hoteli ya Hyatt Regency jijini Dar es salaam leo.

**Tarehe 26/08/2019: Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Mh. Mhandisi Isaack Kamwelwe amehimiza wanasayansi na wataalam wa sekta mbalimbali kuhakikisha wanafanikisha upatikanaji wa mipango madhubuti ya kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa. Alizungumza hayo wakati akifungua rasmi mkutano wa 53 wa utoaji wa utabiri wa Hali ya Hewa wa Msimu wa Mvua za Vuli 2019 "Fifty Third Greater Horn of Africa Climate Outlook Forum" (GHACOF 53) unaofanyika katika Hotel ya Kilimanjaro (Hyatt Regency) kuanzia tarehe 26 hadi 28 Agosti 2019 Dar es Salaam.**

'Naamini baada ya mkutano huu wataalamu mliopo kwenye mkutano huu mtakuja na mpango madhubuti wa kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa ili kuweza kupunguza athari zitokanazo na mabadiliko hayo', alizungumza Mhe. Kamwelwe.

Aidha, Mheshimiwa Kamwele aliwakumbusha wataalam hao kutoka nchi kumi na moja za pembe ya Afrika umuhimu wa kuhusisha utabiri wa jadi (Indigenous knowledge) katika kuboresha utabiri. Alisema kuna wadudu ambao wakionekana inaashiria kuanza kwa mvua na kuna ambao wakionekana inaashiria mvua si za kuridhisha, aliwataka wanasayansi hao kufanya uchambuzi wa kina.

Sambamba na maelekezo hayo, Mheshimiwa Kamwele aliwakaribisha washiriki wa kongamano hilo kutembelea sehemu za vivutio vya utalii vilivyopo hapa nchini na aliwataka kujifunza maneno machache ya Kiswahili.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) na Makamu wa tatu wa Rais wa Shirika la Hali ya Hewa Duniani, Dkt.Agnes Kijazi alimweleza mhe. Waziri kuwa kupitia mikutano hiyo kumekuwa na maboresho makubwa kwenye mfumo wa mawasiliano kati ya wanasayansi na wataalamu kutoka sekta mbalimbali hivyo kusaidia matumizi sahihi ya taarifa za hali ya hewa zitolewazo na taasisi za hali ya hewa za nchi za Pembe ya Afrika.

**INAENDELEA UK 8**





# WAZIRI KAMWELWE AHIMIZA MIPANGO MADHUBUTU YA KUKABILIA NA ATHARI ZA MABADILIKO YA HALI YA HEWA

**INATOKA UK 7**

Pia, Dkt. Kijazi aliishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Mhe. Rais John Joseph Pombe Magufuli kwa kutoa kipaombele katika uboreshaji wa huduma za hali ya hewa hapa nchini.

Aliendelea kwa kusema kuwa uwekezaji unaofanywa na Serikali katika miundombinu ya hali ya hewa ukiwemo mtandao wa rada za hali ya hewa ni kielelezo tosha cha umakini wa serikali kuboresha sekta ya hali ya hewa ambayo ni ya muhimu sana katika kufikia maendeleo endelevu.

Akizungumza kwa niaba ya wakuu wa taasis za hali ya hewa katika nchi za pembe ya Afrika Dkt. Kijazi aliziomba serikali za nchi hizo kuendelea kuboresha huduma za hali ya hewa na pia aliwashukuru ICPAC kwa kuendelea kuendesha makongamano hayo ambayo alisema yameendelea kuwa chachu ya uboreshaji wa utabiri wa msimu katika nchi za pembe ya Afrika.

Kwa upande wa Mkurugenzi wa Taasis inayosimamia Masuala ya Hali ya Hewa kwa Nchi za Pembe ya Afrika (IGAD Climate Prediction and Application Centre (ICPAC)) Dkt. Guleid Artan alielezea lengo la kongamano hilo kuwa ni kujadili na kuandaa kwa pamoja utabiri wa msimu wa mvua za vuli za mwezi Oktoba hadi Desemba 2019, pamoja na kuandaa mikakati ya kukubaliana na hali mbaya ya hewa kwa msimu huo kwa kulenga sekta muhimu za kijamii na kiuchumi ambazo ni pamoja na afya, kilimo na usalama wa chakula, maji, nishati n.k.

Mwakilishi wa Shirika la Hali ya Hewa Duniani, Dkt. Afiesimama aliwajulisha washiriki wa kongamano hilo kwamba katika mkutano wa WMO Congress uliomalizika hivi karibuni Afrika ilifanikiwa kuwa na mwakilishi katika ngazi za juu za uongozi wa Shirika hilo kupitia Dkt. Agnes Kijazi, Mkurugenzi mkuu wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania ambaye alichaguliwa katika nafasi ya Makamu wa tatu wa Rais wa WMO. Aidha, aliahidi kwamba WMO itaendelea kuzisaidia nchi wanachama kuboresha huduma zikiwemo nchi za pembe ya Afrika.

Wengine waliozungumza katika ufunguzi wa Kongamano hilo ni mwakilishi wa Bank ya maendeleo ya Afrika Dkt. Solomon Ngoze ambae alielezea misaada mbali mbali iliyotolewa na Bank hiyo katika kuboresha huduma za hali ya hewa kwenye nchi za pembe ya Afrika. Mwakilishi wa programu ya WISER Mr. Adam Curtis alielezea mafanikio yaliyofikiwa katika kutekeleza programu hiyo. Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Dkt. Buruhani Nyenzi aliwakumbusha washiriki hao kwamba kongamano la kwanza lilifanyika nchini Zimbabwe mwaka 1996 ambapo yeye binafsi alikuwa kiongozi wa taasisi iliyohusika na ukame kusini mwa Afrika ambayo ndiyo iliendesha kongamano hilo. Alionyesha furaha yake kuona kwamba makongamano hayo yanaendelea kwa ufanisi mkubwa.

**GHACOF ni Mkutano unaojumuisha nchi za Pembe ya Afrika ambazo ni Tanzania, Kenya, Somalia, Ethiopia, Sudan, Sudan ya Kusini, Uganda, Burundi, Rwanda, Djibouti na Eritrea pamoja na mashirika ya Kimataifa ikiwemo Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO).**



# HALI YA HEWA: WATUMIAJI WA ZIWA VIKTORIA KUNUFAIKA




**Tarehe 18/07/2019:** Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeandaa mpango maalumu wenye lengo la kuongeza ufanisi wa utoaji wa tahadhari za hali mbaya ya hewa kwa watumiaji wa Ziwa Viktoria. Mpango huo ulibainishwa wakati wa uzinduzi rasmi wa mradi wa 'HIGH impact Weather lAke sYstem (HIGHWAY)' uliofanyika katika ukumbi wa mkutano wa Ubungo Plaza na Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TMA Dkt. Ladislaus Chang'a .

'Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imedhamiria kuongeza ufanisi wa uandaaji na usambazaji kwa wakati wa taarifa za hali ya hewa hususani taarifa za hali mbaya ya hewa kwa watumiaji wa Ziwa Viktoria', alibainisha Dkt. Chang'a.

Aliongezea 'wadau wa mradi huu wakiwemo wataalam kutoka TMA watakaa pamoja na kufanyia maboresho taarifa zinazoatolewa na Mamlaka na hivyo kufanikisha utoaji wa huduma bora zaidi na kusaidia serikali katika jitihada za kuhakikisha huduma za hali ya hewa nchini zinachangia katika kufanikisha mikakati na jitihada za nchi kufikia uchumi wa kati na uchumi wa viwanda ,'

Awali wakati wa ufunguzi, Bi. Rita Roberts mtaalam wa mradi kutoka 'National Centre for Atmosphere Research (NCRA)' alifafanua kuwa mradi huu utasaidia Kanda ya Afrika Mashariki kupitia taasisi zake za hali ya hewa kufanikisha utoaji endelevu wa tahadhari za hali mbaya ya hewa kwa wakati pamoja na kuongeza kiwango cha usahihi na uhakika kwa taarifa za hali ya hewa na hivyo kupunguza athari za vifo na upotevu wa mali.

Mradi huu unahusisha Taasisi za Hali ya Hewa za Tanzania, Kenya, Uganda na Rwanda kwa kushirikiana na Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO) na 'National Centre for Atmosphere Research (NCRA)' kutoka Marekani, Taasis ya Hali ya Hewa ya Uingereza (UKMet Office) kwa ufadhili wa 'Department for International Development (DFID)' ya Uingereza.



ISO: 9001 2015 Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga
Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA)

# BODI YAMPONGEZA DKT. KIJAZI KUCHAGULIWA MAKAMU WA TATU WA RAIS WA **WMO**



**Bodi ya Ushauri ya Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA) imempongeza Dkt. Agnes Kijazi, Mkurugenzi Mkuu wa TMA na katibu wa hiyo kwa kuchaguliwa kwa kishindo kuwa makamu wa tatu wa Rais wa Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO).**

Akizungumzia pongezi hizo na ushindi uliopatikana wakati wa kikao cha 55 cha Bodi, mwenyekiti wa Bodi Dkt. Buruhani Nyenzi aliwasilisha pongezi za dhati kutoka kwa wajumbe wote na kukiri kuwa nafasi iliyopatikana ni moja ya njia za kuzidi kuipandisha Tanzania juu katika anga za kimataifa.

‘Bodi inatoa pongezi za dhati kwa Dkt. Kijazi kwa kuchaguliwa kushika nafasi ya juu WMO, kwa kuwa kupitia nafasi hiyo Tanzania inazidi kupanda juu katika anga za kimataifa’. Aliongea Dkt. Nyenzi

Mwenyekiti huyo aliendelea kuwakumbusha washiriki wa kikao hicho kuwa mafanikio ambayo Tanzania imeyapata yanachangiwa na mambo mengi. Alisema jambo la kwanza na la muhimu ni sifa za Dkt. Kijazi kama mgombea wa nafasi hiyo, pili kukubalika na kukua kwa diplomasia ya Tanzania nje ya nchi na tatu sifa nzuri za Watanzania ambao wamewahi kufanya kazi WMO akiwemo yeye mwenyewe.



Aidha, Dkt. Nyenzi alionesha furaha yake namna ambavyo TMA inafanya kazi kwa umoja na upendo baina ya wafanyakazi, akitolea mfano mapokezi yaliyofanywa na wafanyakazi kwa kiongozi wao ambaye ni Dkt. Kijazi.

Dkt. Kijazi alichaguliwa kuwa makamu wa tatu wa Rais wa WMO kwenye mkutano wa 18 wa shirika hilo uliofanyika jijini Geneva, Uswisi tarehe 03-14 Juni 2019 kwa kipindi cha miaka minne, akiwa mwanamke na makamu wa tatu wa Rais wa kwanza kutoka nchi zinazoendelea hususani nchi za Afrika zilizo kusini mwa jangwa la Sahara.

# TUJITATHIMI MAPUNGUFU YETU NA KUBORESHA UTENDAJI KAZI - DKT. KIJAZI

**25/06/2019**
Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) imefanya kikao cha wafanyakazi kilichofanyika katika ukumbi wa mikutano wa TMA kwa kujumuisha wafanyakazi kutoka Makao Makuu na Ofisi ya Kituo Kikuu cha Utabiri (CFO).

Akizungumza katika kikao hicho, Mkurugenzi Mkuu wa TMA, Dkt. Agnes Kijazi ambaye ndiye aliyekuwa mwenyekiti wa kikao hicho, aliwataka wafanyakazi kujitathimini mapungufu yaliyopo ili kuboresha utendaji wa kazi za Mamlaka.

'Ili kuboresha huduma zetu kama Mamlaka na kukidhi matakwa ya sheria mpya ya huduma za hali ya hewa nchini, tunatakiwa tujitahimini wenyewe mapungufu yetu ili tuweze kuboresha utendaji kazi wetu'.Alizungumza Dkt. Kijazi.

Aliendelea kwa kusisitiza bidii na weledi mahali pa kazi ili kuongeza ufanisi wa kazi za Mamlaka na kutambua kuwa jukumu letu ni kuhudumia wananchi wanaoitegemea TMA katika utoaji wa huduma za hali ya hewa. Aidha Dkt. Kijazi aliwakumbusha wafanyakazi kuhusiana na kuvaa mavazi sahihi kulingana na taratibu za ofisi za umma pamoja na wale wanaohitaji huduma kutoka nje ya Mamlaka.

Dkt. Kijazi alitumia nafasi hiyo kuwashukuru wafanyakazi wote kwa ushirikiano na upendo waliouonesha katika mchakato mzima wa uchaguzi wa kuwania nafasi ya umakamu wa tatu wa Rais wa WMO na mapokezi ya heshima kwake.

Menejiment ya TMA imeweka utaratibu wa kukutana na wafanyakazi wa Mamlaka ili kujadilia masuala mbalimbali ya uboreshaji wa huduma zake sambamba na kutatua changamoto zinazoweza kujitokeza katika kipindi husika. Mwenyekiti wa vikao hivyo ni Mkurugenzi Mkuu wa TMA.











# Maswali na majibu


## Sheria mpya ya hali ya hewa inaongeza chachu gani katika majukumu ya TMA?

Sheria ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania pamoja na jukumu la kutoa huduma za hali ya hewa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeiongezea Mamlaka majukumu kwa mujibu wa Sheria Na. 2 ya 2019 ikiwa ni pamoja na jukumu la:

•Kudhibiti masuala ya hali ya hewa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa nia ya kuhakikisha miongozo yote muhimu ya kitaifa na kimataifa kuhusu uwekaji wa vituo vya hali ya hewa nchini vinazingatiwa ili kupata takwimu bora zaidi kwa manufaa ya wadau wa hali ya hewa na Taifa kwa ujumla. Udhibiti huo pia utasaidia kuwepo kwa matumizi sahihi ya rasimali zilizopo nchini na kupunguza madhara yatokanayo na uwekaji vifaa na vituo vya hali ya hewa usiozingatia miongozo hiyo muhimu na hivyo kukosa tija kwa Taifa;

•Kuratibu vituo vya hali ya hewa vinavyomilikiwa na Sekta za Umma na Sekta Binafsi katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kuwezesha wadau hao kubadilishana mawazo kwa nia ya kuboresha sekta ya hali ya hewa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kushirikiana katika uwekaji wa vituo, vifaa na mitambo ya hali ya hewa katika Jamhuri ya Muungano, hivyo kuwezesha kuwepo kwa matumizi sahihi ya rasilimali fedha na vifaa/mitambo ya hali ya hewa kwa kuwepo kwa mtawanyiko mzuri wa vituo vya hali ya hewa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Aidha, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania itaendelea kushirikiana na wadau wa Sekta ya Umma na Binafsi katika kutekeleza majukumu yake ya kisheria kwa uweledi na ufanishi mkubwa ili kuwa na tija zaidi na ili hali ya hewa iendelee kutoa mchango mkubwa zaidi katika kuwezesha Tanzania kuelekea kwenye uchumi wa kati (Uchumi wa Viwanda) kama ilivyo mikakati ya serikali na kupunguza athari zitokanazo na hali mbaya ya hewa.




*• Nishati: Taarifa za hali ya hewa kama vile nguvu na mwelekeo wa upepo, nguvu na vipindi vya jua, hali ya mawingu, kiasi cha mvua husaidia kumwezesha mwekezaji kuwekeza aina ya nishati katika eneo husika.*

# MATUKIO MBALIMBALI KATIKA PICHA

## MAPOKEZI YA DKT. KIJAZI JNIA NA MAKAO MAKUU













# MATUKIO MBALIMBALI KATIKA PICHA MAONESHO YA SADC NA NANENANE















# MATUKIO MBALIMBALI KATIKA KAMPENI YA KUTANGAZA VIVUTIO VYA UTALII WA TANZANIA NA KUGOMBEA NAFASI YA MAKAMU WA TATU WA RAIS WA SHIRIKA LA HALI YA HEWA DUNIANI (WMO)







Na. William Shechambo

# SAYANSI, TEKNOLOJIA KUTHIBITISHA UMWAMBA KADA YA UTABIRI WA HALI YA HEWA

TAALUMA ya Utabiri kama zilivyo taaluma zingine duniani, inahitaji ufahamu wa kwenda shuleni na kuingia darasani, ambapo mwanataaluma hulazimika kufaulu masomo fulani, ambayo kwa kada hii, lazima yawe ya sayansi.

Kimsingi masomo ya sayansi kwa maana ya Fizikia, Baiolojia, Kemia, Jiografia na Hesabu, ndio hasa msingi wa teknolojia kwa sababu mababa wa teknolojia nyingi, ukifuatilia vizuri utabaini kitaaluma ni wanasayansi.

Nikiwataja kwa uchache, Douglas Engelbart, alikuwa bingwa wa kompyuta; Norman Abramson na yeye alikuwa mchawi kwenye teknolojia ya 'Wireless' yaani muunganiko wa kiteknolojia usiohitaji waya, Jack Nilles; Marty Cooper, Gerald Lawson, Nathaniel Borenstein na Robert Metcalfe, hawa wote huwezi kuwaacha ukichimbua historia ya teknolojia na wote ni wana sayansi.

Kwa mantiki hiyo, utakubaliana na mimi kuwa sayansi ndio msingi wa teknolojia duniani na ndio sababu utabiri wa hali ya hewa ambao kwa kiasi kikubwa unatumia vifaa vyenye teknolojia ya hali ya juu, unahitaji umakini na hufanywa na wanasayansi makini ili kuleta matokeo sahihi kwa wakati sahihi.

Robert FitzRoy, ukimtaja kwenye ulimwengu wa watabiri utaonekana miongoni mwa wataalamu hao kwa sababu mpaka sasa, Muingereza huyu anatajwa kuwa mwanasayansi wa kwanza kufanikiwa kutabiri mabadiliko ya hali ya hewa akiwa kama Nahodha wa chombo cha majini kilichoitwa HMS Beagle, kwenda Tierra del Fuego, Amerika ya Kusini.

Historia ya muasisi huyu wa utabiri ilikwenda mpaka karne hii ya 21, karne ya sayansi na teknolojia ambayo kumefanyika ubunifu mkubwa wa kila nyanja huku ukipewa nguvu na maendeleo ya teknolojia.

Moja ya sehemu zilizopata mafanikio ni kada ya utabiri wa hali ya hewa, ambayo kutoka matumizi ya vifaa vya hali ya chini, mpaka kutumia mitambo ya kisasa na yenye mifumo mizito ya kompyuta, utabiri umekuwa rahisi na sahihi kwa kiasi kikubwa.

Hapa nchini, serikali imefahamu umuhimu wa utabiri wa hali ya hewa ambao ni kama taarifa za angalizo zinazoweza kuokoa maisha ya mamilioni ya watu, ndio sababu ikaamua kuwezesha Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA), katika nyanja za utumishi na vifaa.

Teknolojia licha ya kuwa gharama haidanganyi, kwa sababu tangu TMA iwezeshwe kirasilimali, kwa mujibu wa Mkurugenzi Mkuu, Dk. Agnes Kijazi, ufanisi wao kwenye utabiri unazidi kupanda, mwaka hadi mwaka.

Hivi karibuni, nilifuatilia kikao kimoja nyeti, ambacho kiliwashirikisha wanasayansi wa hali la hewa nchini ambao walikutana ili kuandaa mwelekeo wa hali ya hewa kwa msimu wa vuli yaani Oktoba hadi Desemba (OND).

Katika mkutano huo ambao ni dhahiri ulikutanisha vichwa vya sayansi, ili kukamilisha maandalizi ya kutoa utabiri au mwelekeo wa msimu huo wa mvua za vuli, wataalamu hao walijadili rasimu ya kazi waliyoifanya kwa muda sasa.

Dk. Kijazi akiongoza kikao hicho, aliwataka wataalamu hao kuandaa kwa pamoja na kupitia mfumo mzima wa uaandaaji ili kujiridhisha  na utabiri utakao tolewa siku chache zijazo sambamba na kutoa mapendekezo ya uboreshaji katika maandalizi mengine ya misimu ijayo.

Mtaalamu huyo, ambaye ni kati ya wanawake kadhaa nchini wanaothibitisha kuwa mwanamke akiamua anaweza, alitumia nafasi ya mkutano huo kuwapongeza wanasayansi hao kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kutoa utabiri wenye viwango vya juu vya usahihi kwa zaidi ya asilimia 80.

Kimsingi pongezi hizo zinatoa motisha wa wataalamu wetu ambao amewataka kufanya kazi kwa bidii na ushirikiano ili kufikia ufanisi wa juu ya asilimia 90 kwa sababu vifaa vipo tena vya kisasa na vyenye teknolojia kubwa.

Taarifa niliyoipata kwenye mkutano huo ni kwamba hii ni mara ya kwanza kwa TMA kuwakutanisha wanasayansi kutoka vituo vyote vya utabiri nchini, ambapo awali kazi ya uandaaji utabiri ilikuwa ikifanywa na wanasayansi wa ofisi ya makao makuu na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA).

Baada ya mkutano huo, imeelezwa kuwa mwelekeo wa msimu wa mvua za vuli kwa mikoa inayopata mvua mara mbili kwa mwaka, utatangazwa wiki ya kwanza ya Septemba yaani Septemba 6, mwaka huu, hivyo ni matumaini yangu kwamba ufanisi wa utabiri kwa msimu ujao utavunja rekodi.

Nimesema hivyo kwa sababu kama mababa wa utabiri waliweza kusema mvua itanyesha leo kwenye baadhi ya maeneo ya sehemu fulani, na wakati huo walikuwa hawana teknolojia lakini walikuwa wakipatia kwanini leo tushindwe wakati tuna watu vichwa wa sayansi na teknolojia inatubeba?

Taarifa sahihi za utabiri wa hali ya hewa, zinazotolewa kwa wakati sahihi huokoa maisha na mali.



# TMS KUWAJENGEA UWEZO WADAU MATUMIZI SAHIHI YA TAARIFA ZA HALI YA HEWA NCHINI.

**Chama cha Wataalam wa Hali ya Hewa Tanzania (TMS) kwa kushirikiana na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) kupitia mradi wa "Weather and Climate Information Services" (WISER), WISER, kiliweza kuwajengea uwezo wadau wa sekta mbalimbali (Kilimo, ufugaji, nishati, maafa, maji pamoja na wanahabari) katika halmashauri za miji ambazo ni Kongwa, Dodoma mjini, Hanang' na Babati kwa kuendesha mafunzo ya matumizi sahihi ya taarifa za hali ya hewa kuanzia tarehe 27 Mei mpaka 31 Mei 2019.**



Wageni rasmi katika mafunzo hayo, walikuwa ni wakurugenzi wa halmashauri za miji ambao katika hotuba zao waliishukuru TMS kwa kuchagua kufanya mafunzo hayo muhimu katika halmashauri zao. Aidha, wageni rasmi walihamasisha kila mshiriki kupitia taaluma zao kuitumia vyema fursa hiyo adhimu waliyoipata kwa kutambua namna ya kupata taarifa za hali ya hewa, kuzielewa kwa usahihi na pia kuzifikisha kwa walengwa kwa wakati zitakazoimarisha mchango wa sekta ya hali ya hewa katika kuongeza tija na ufanisi kwenye kilimo ambacho kina mchango mkubwa wa kuzalisha malighafi kwa ajili ya Tanzania ya viwanda hivyo utekelezaji wa programu hii utachangia katika kuunga mkono juhudi za Mh. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania dkt. John Pombe Magufuli za kulifikisha Taifa katika uchumi wa kati na uchumi wa viwanda.

Kwa upande wa washiriki walikiri kupata uelewa kwa kiasi kikubwa na kuahidi kuhakikisha taarifa za hali ya hewa zinatumika kwa usahihi na kusambazwa kwa wakati ili kuwafikia walengwa pamoja na kuweka nguvu kubwa katika kushirikiana na TMA.

Malengo ya mafunzo hayo ni kuchochea matumizi ya taarifa za hali ya hewa kwa sekta mahsusi zilizoainishwa katika mradi wa WISER na kuwafikia wananchi wengi kupitia huduma ya taarifa za hali ya hewa inayotolewa kwa njia ya simu za mikononi uitwao FarmSMS, ambapo zaidi ya wadau 600 walisajiliwa katika mfumo huo.

